



TANGAZO KWA UMMA

MIKATABA YA UNUNUZI WA MAHINDI MEUPE (NON-GMO), MTAMA MWEUPE NA MPUNGA

Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ni Taasisi ya Serikali chini ya Wizara ya Kilimo. NFRA imeanzishwa chini ya Sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 ya mwaka 1997 kwa madhumuni ya kuhakikisha usalama wa chakula Nchini. Katika kutekeleza moja ya majukumu yake, NFRA hahunuma nafaka kwa ajili ya Akiba ya Taifa ya chakula.

NFRA inatarajia kununua Mahindi Meupe, Mtama Mweupe na Mpunga katika msimu wa ununuzi wa mwaka 2026/2027, kuanzia tarehe 1 Julai, 2026. Ununuzi huo utafanyika kwenye maghala ya Wakala yaliyopo kanda za Arusha (ghala la Arusha na Babati), Dodoma (ghala la Dodoma Mjini, Mtanana na Manyoni), Kipawa (Dar es Salaam), Makambako, Songwe, Shinyanga, Songea, Sumbawanga na Mpanda, na katika vituo vingine ambavyo vitafunguliwa na Wakala pindi zoezi la ununuzi litakapoanza.

Aidha, ili kuongeza wigo wa kufikia ununuzi wa tani zaidi ya 1,200,000 za nafaka tajwa pamoja na kuwahakikishia Vikundi vya Wakulima (AMCOS), Wakulima Wakubwa na Wafanyabiashara soko la uhakika la nafaka, NFRA inapokea maombi na kuingia Makubaliano (Framework Agreement) ya Ununuzi wa nafaka na waombaji wenye sifa na wanaokidhi masharti yaliyoainishwa hapa chini.

1. MASHARTI KWA KIKUNDI CHA WAKULIMA (AMCOS):

- Cheti cha Usajili wa Kikundi (AMCOS);
- Namba ya Mlipa Kodi (TIN);
- Leseni ya biashara ya mazao ya chakula/nafaka iliyohai; na
- Barua ya maombi iliyoainisha jina na anuani ya mwombaji, namba ya simu, baruapepe, kiasi cha Mpunga/Mtama Mweupe/Mahindi Meupe anayokusudia kuuzia NFRA na kituo cha NFRA anachopendekeza kuwasilisha nafaka yake.

2. MASHARTI KWA MKULIMA MKUBWA:

- Uthibitisho wa uraia au usajiri wa kampuni iliyosajiliwa Tanzania;
- Mkulima awe na shamba kuanzia ekari 100 ndani ya eneo moja katika Halmashauri/Wilaya na kuwasilisha barua ya uthibitisho huo kutoka Serikali ya Kijiji/Halmashauri ya Wilaya shamba lilipo;
- Mkulima awe na uwezo wa kuzalisha kuanzia tani 200 za Mahindi Meupe/Mpunga au tani 50 za Mtama Mweupe;
- Namba ya Mlipa Kodi (TIN);
- Leseni ya biashara ya mazao ya chakula/nafaka iliyohai; na
- Barua ya maombi iliyoainisha jina na anuani ya mwombaji, namba ya simu, baruapepe, kiasi cha Mpunga/Mtama Mweupe/Mahindi Meupe anayokusudia kuuzia NFRA na kituo cha NFRA anachopendekeza kuwasilisha nafaka yake.

3. MASHARTI KWA MFANYABIASHARA:

- Uthibitisho wa uraia au usajiri wa kampuni iliyosajiliwa Tanzania;
- Awe na uwezo wa kuuzia NFRA kuanzia tani 2,000 za Mahindi Meupe/Mpunga au tani 50 za Mtama Mweupe;
- Namba ya Mlipa Kodi (TIN);
- Hati hai ya kutodaiwa kodi (valid Tax Clearance Certificate);
- Leseni ya biashara ya mazao ya chakula/nafaka iliyohai; na
- Barua ya maombi iliyoainisha jina na anuani ya mwombaji, namba ya simu, baruapepe, kiasi cha Mpunga/Mtama Mweupe/Mahindi Meupe anayokusudia kuuzia NFRA na kituo cha NFRA anachopendekeza kuwasilisha nafaka yake.

MASHARTI YA JUMLA

Mwombaji anapaswa kuwa na:

- Utayari wa kuridhia kuuza nafaka yake kwa bei itakayopangwa na NFRA;
- Utayari wa kuridhia kuwasilisha Mahindi Meupe, Mtama Mweupe au Mpunga katika ghala/kituo atakachoelekezwa na kwa muda atakaopangiwa kwa mujibu wa Makubaliano atakayoingia na NFRA;
- Mahali salama pakuhifadhi Mpunga, Mtama Mweupe au Mahindi Meupe kabla ya kununuliwa na NFRA; na
- Mpunga, Mtama Mweupe au Mahindi Meupe ya daraja la kwanza yenye kuzingatia vigezo vya ubora kama vilivyowekwa na NFRA kwa mujibu wa viwango vya Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Tanbihi: Kikundi/Mkulima/Mfanyabiashara asiye na vigezo tajwa hapo ataendelea kuuza nafaka zake kwa kuwasilisha katika maghala makuu ya NFRA yaliyopo katika Ofisi za Kanda au vituo vya ununuzi vitakavyofunguliwa na NFRA, pasipo kuwa na Makubaliano ya ununuzi kutoka NFRA.

4. NAMNA YA KUTUMIA MAOMBI:

Mwombaji anaelekezwa kuwasilisha maombi yake ya kuuzia NFRA Mpunga, Mtama Mweupe au Mahindi Meupe katika mfumo wa **Digital Food Tracking System** (DFTS) unaopatikana kupitia tovuti ya www.dfts.nfra.go.tz/ui/auth. Kufikia tovuti husika unaweza kutumia msimbo (QR Code) hii hapa.



Kufahamu namna ya kutumia mfumo kuwasilisha maombi yako fuata maelekezo yaliyo katika msimbo (QR Code) hii hapa.



Kwa taarifa zaidi Mwombaji anaweza kuwasiliana na NFRA kupitia simu namba **+255 (0) 26 2963953; +255 718471330; +255 612899780** au Baruapepe: info@nfra.go.tz

Imetolewa na:

Afisa Mtendaji Mkuu,

Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula

Tarehe 01 Aprili, 2026.